# Aina Za Uongozi

Muhtasari huu unatuambia majibu yako ya maswali ili kukupima ni jinsi gani unatosha katika aina sita tofauti za uongozi.**Hakuna hata aina moja ilivo na umuhimu au upungufu kuliko nyingine-zinakamilishana na kutogemeana moja kwa nyingine,** - Kwa uwazi zaidi, taarifa hii inategemea majibu yako. Kwa kila eneo majibu yako yameunganishwa pampja ili kutoa jumla iliyo katika ya alama 5 na 25, ambapo alama 25 zinamaanisha kuwa wewe ni imara sana katika eneo hilo, naalama 5 zinasimama katika eneo la udhaifu wako. Kitu cha muhimu ni kuangalia alama katika maeneo husika. Chukuwa muda wa kumsifia na kumshukuru Mungu katika maeneo uliyo imara katika uonogozi. Vile vile utahitaji kuomba ili kujua ni mtu gani aliye mzuri katika maeneo yako ya udhaifu. Kama haya matokeo ya muhtasari huu yamekushangaza, mshirikishe mtu mwingine wa karibu anayekujua vizuri-inaweza kuwa tu ni swali moja au mawili au tafsiri ya maswali hayo kilichoathili alama zako.

Hamishia alama zako sas katika jedwari hapa chini, ukimbuka kutoa alama ulizopatia maswali yaliyotolewa katika mstari wa mwisho wa jedwari. Hivyo kila eneo litakuwa na alama. Baadhi ya watu watafanana kwa zaidi, wengine watakuwa na tofauti-hii inafuatana na jinsi ulivyogawa alama.

| Uongozi wa Utangulizi | Uongozi wa Mbinu | Utawala | Uongozi wa Timu | Uongozi wa Kichungaji | Uongozi wa Faraja |
|---|---|---|---|---|---|
| Q1 | Q8 | Q2 | Q6 | Q7 | Q3 |
| Q11 | Q10 | Q9 | Q12 | Q14 | Q5 |
| Q20 | Q16 | Q18 | Q25 | Q22 | Q13 |
| Q26 | Q28 | Q24 | Q30 | Q29 | Q19 |
| Ongeza 6 | Ongeza 6 | Ongeza 6 | Ongeza 6 | Ongeza 6 | Ongeza 6 |
| Jumla | Jumla | Jumla | Jumla | Jumla | Jumla |
| - Q4 | - Q21 | - Q15 | - Q23 | - Q17 | - Q27 |
| | | | | | |

**Uongozi wa Utangulizi**. (q1+q11+q20+q26+(6-q4))
Viongozi wa utangulizi ni watu ambao wako tayari kujitupa wenyewe, bila kujali hatari yote inayoweza kujitokeza mbele yao, wakisonga mbele ili kugundua na kufikia malengo ya kihuduma, “wakiyasahau yaliyonyuma, wakiyachuchulilia yaliyo mbele.” (Filp. 3:13)
Viongozi hawa huwa na moyo na maono, na wamejitoa kuyatimiza. Paulo ni mfano mzuri wa viongozi wa utangulizi akiwa na lengo la kuipanua mipaka ya kanisa, richa hatari ya maisha yake ya binafsi. Viongozi hawa wanakuwa na nguzu zaidi katika hatua zao za kwanza katika kazi, wakifurahia popote Mungu anapowaitia. Kadri muda unavyopitra hupungukiwa na ile hali ya utekelezaji wa maono. Kwa hamu wakiangalia mbele kwa changamoto nyingine.

**Uongozi wa Mbinu.** (q8+q10+q16+q28+(6-q21))
Viongozi walio na uwezo wa kugawanya maono na malengo yao makubwa katika sehemu ndogo ndogo katika uwezo wa kiutendaji ni wa muhimu kwa kanisa. Viongozi wa mbinu wana ufahamu na mwelekeo wa kuunda njia za kuyafikia maono, na wana uwezo wa kuwashawishi watu wengine wa kanisa kukubali mpango wake. Nehemia alipowaongoza Wayahudi katika ujenzi wa kuta za Yerusalemu, alionyesha hali ya juu ya aina hii ya uonggozi kwa kuigawa kazi, na katika kuifanya kazi vile ingefaa kufanyika. Mpango wake ulikuwa mzuri, kuta zilijengwa katika muda wa siku 52.

This material is copyright to The Teal Trust ( www.teal.org.uk ) © 2001. It may be reproduced for non-profit use providing copyright attribution is kept.

Viongozi wa mbinu huleta hali fulani katika ufahamu wa kawadia. Kama watangulizi hata hivyo, wanaweza kupoteza mori katika utekelezaja wa kazi, wakipendelea kuachia kazi hii kwa wengine.

**Utawala** - (q2+q9+q18+q24+(6-q15))
Makanisa yote yanahitaji watumishi na wakurugezi, watu wenye vipaji vya utawala (Mdo. 6). Maono na mabadiliko yoyote yatahitaji watu wenye uwezo wa kupanga na katatua matatizo, kugawa majuku na kukusanya. Bila kipawa hiki, maono mazuri hayawezi kutekelezwa! Mitume walitoa majukumu ya kugawa chakula cha ushirika na kuwahudumia wajane kwa wale waliokuwa na kipaji na ujuzu wa kimsingi, ikiwa ni pamoja na Stefano na Filipo. Wakurugenzi mara nyingi wanasifa kidogo, kwa sababu ya aina ya kazi yao isiyoonekana sana kama zingine. Hata hivyo kazi nyingi isingeweza kufanyika bila wao. Wanaweza kuwa na bidii kama ya watangulizi-lakini kwawana ndoto ya kufanya yasiyowezekana.

**Uongozi wa Timu.** (q6+q12+q25+q30+(6-q23))
Ufunguo wa nguvu za viongazi wa timu ni kiu ya kufanya kazi na wengine, na uwezo wa kuwatumaini. Viongozi wa timu wanahitaji kujishusha kwa hali ya juu na hali ya utumishi-lengo lao kuu ni kuona timu imeyafikia malengo yake. Kuyafikia malengo ya binafsi ni kitu kinachofuata. Mchango mkuu wa Sila alioutoa kwa kanisa labda ni kufundisha na kuimarisha huduma ya Paulo ili aweze kufikia mambo mengine makuu zaidi baadaye. Viongozi wa timu hawana faida-ikiwa kanissa litafanya kazi kama mwili, viongozi wa timu hulinda umoja na ufanisa katika njia zitumiwazo na timu kufanya kazi.

**Uongozi wa Kichungaji** - (q7+q14+q22+q29+(6-q17))
Viongozi wengi wa kanisa hujisikia kwamba wangekuwa uongozi wa kichungaji kama aina yao ya msingi wa uongozi. Hii haimaanishi kuwa si wachungaji wanaosaidia, bali ni kwamba aina yao ya uongozi iko katika eneo tofauti na mazingira ya uongozi. Viongozi wa kichungaji ni watu wa watu, walio na sehemu muhimu katika kuwategemeza watangulizi, wanambinu, viongozi wa timu, na washirika wote wa kanisa, hasa hasa wakati wa ugumu. Maono na kuisgia katika maono huonekana kuwa na umuhimu mdogo kwa viongozi wa kichungaji. Petro alikuwa ni kiongozi wa kichungaji, kinyume na kazi ya Paulo ya upandaji makanisa na mausia yake. Uongozi wa kichungaji mara nyingi hauonekani, na mara nyingi hausifiwi hadharani, ijapkuwa ni wa muhimu sana. Wale ambao ni viongozi wa kichungaji wanaweza kuogopeshwa na watanguluzi na wanambinu-na wakati mwingine kusumbuliwa na mipango ya wakurugenzi. Pamoja na hayo mchango wao si wa faida-chukuwa muda ufikirie juu ya kiongozi wa kichungaji-na utaona kuwa labda wanataka heshima na msaada mkubwa.

**Uongozi wa Faraja.** (q3+q5+q13+q13+(6-q27))
Paulo alikuwa ni mfariji mkuu-barua zake kwa makaniza ya kwanza zilikuwa na mausia, taraja, na mafundisho. Viongozi wafariji wanaweza kuyainua makanisa, timu, na hata watu binafsi. Wana ufahahamu mkubwa juu ya vipawa vya waty, hisia zao, na ni kitu gani cah kuwainua, ili kuwasaidia katika kuvitumia katika huduma zao. Ni nani asiyehitaji faraja!! Viongozi wafariji wana ustadi wa kujua ni wakati gani neno halisi liwezalo kuwawasha watu moto wa kusonga mbele, kujua lini kutoa changamoto na lini kutegemeza, lini kufundisha na lini kutoa nafasi. Kwa kipindi wanaweza kuwaudhi watu kwa kutokutoa msaada zaidi na faraja tofauti na aina nyingine za uongozi-wakati mwingine watu hutaka zaidi ya faraja tu.

The Teal Trust
This material is copyright to The Teal Trust ( www.teal.org.uk ) © 2001. It may be reproduced for non-profit use providing copyright attribution is kept.